**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Shule ya Sekondari Kirando**
**S.L.P 107**
**NAMANYERE-NKASI**
**Tarehe 01.05.2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ............**
**..................................................**
**S.L.P .........................................**
**..................................................**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIRANDO HALMASHAURI YA NKASI MKOA RUKWA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya __________(Aliyopangiwa ).

Shule ya Sekondari Kirando ipo umbali wa Kilometa 63 Magharibi mwa Mji wa Namanyere Usafiri wa basi kutoka mjini Sumbawanga/Namanyere unapatikana katika kituo cha mabasi Sumbawanga na Namanyere Nauli ni Shilingi **10,000/=** kutoka Sumbawanga na Shilingi **6,000/=** kutoka Namanyere kwa basi,Anayetokea Mpanda ashukie Namanyere.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ...........( Iliyotangazwa na serikali ) hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe tajwa, Mwisho wa kuripoti ni wiki mbili tu kuanzia tarehe pangwa na serikali.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni sketi mbili nyeusi na blue bahari mpauko
ii. Mashati mawili meupe mikono mirefu.
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.
iv. Sare ya Michezo Kwa wasichana ni truck suti rangi ya blue.
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi jozi mbili nyeupe
vii. Sweta rangi ya blue bahari mpauko (*siyo lazima kuna joto)*
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) *rangi damu ya mzee drafuti ndogo mshono wa solo.*
ix. Tai mbili zenye kufanana na sketi yaani nyeusi na blue bahari mpauko
x. T-shirt rangi ya blue muundo wa form six yenye kola nyeupe

**MUHIMU : MAVAZI YOTE NUNUA HUKOHUKO AJE NAYO.**

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari 07 ( Counter book 2Q )
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iv. Godoro la kiwanafunzi futi 2.5
v. Mashuka Jozi 2 rangi ya pink, blanket nyepesi 1 au shuka zito
vi. Chandarua 1
vii. Nguo za dharura ( kitenge 1 na kanga 1 )
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko kwa matumizi yake mwenyewe.
x. Kwanja 1 na Mfagio wa brash **( HGL NA HGFA )**
xi. Jembe 1**, ( HGK )**
xii. Reki 1, **( HKL )**

## 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Fedha hii iwekwe kwenye akaunti ya shule**
**DEVELOPMENT KIRANDO SECONDARY SCHOOL**
**62001100059**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;

xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule** ...........................................

**Jina la Mkuu wa Shule** ERNEO C. MGINA

**Mhuri wa Mkuu wa Shule** MKUU WA SHULE SHULE YA SEKONDARI KIRANDO S.L.P 107, NAMANYERE NKASI

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0754-530654 / 0624530654 / 0737951172 / 0684829104**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0766183759**

- **Mwandamizi malezi (Matron ) 0762845392**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI**
**YA RAIS - TAMISEMI**
**SHULE YA SEKONDARI KIRANDO**

## FOMU YA KUTHIBITISHA AFYA.

*(Fomu hii inajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali na kurudishwa kwa mkuu wa shule ya sekondari NKASI*

*Jina la mwanafunzi.............................................................................*

*Tafadhari naomba kwamba uweze kumpima hali yake ya afya mwanafunzi mwenye jina hapo juu ili kumthibitisha kiasi chake cha afya kuweza kumdu shughuli za masomo darasani, kazi za mikono na michezo. Tafadhari weka alama ya ve (√) mbele ya eneo alilopimwa / kuchunguzwa kwenye neon HAPANA au NDIYO na iwapo ni NDIYO kwamba limeoonekana tatizo basi eleza katika nafasi iliyowekwa.*

*J e, mwanafunzi ana tatizo lolote katika sehemu zifuatazo?*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Uwezo wa kuona: MACHO | HAPANA..............NDIYO............ | .......... |
| 2 | Uwezo wa kusikia | HAPANA............. NDIYO............ | .......... |
| 3 | Uwezo wa kusema: sauti | HAPANA............. NDIYO............ | .......... |
| 4 | Kifua kikuu TB | HAPANA............. NDIYO............ | .......... |
| 5 | Shinikizo la damu | HAPANA............. NDIYO............ | .......... |
| 6 | Ulemavu wa viungo | HAPANA............ .NDIYO............ | .......... |
| 7. | Tatizo lolote la kiafya | HAPANA............. NDIYO............ | .......... |
| 8 | Akubaliwe kupokelewa kusoma | HAPANA...........NDIYO............ | .......... |

9. *Kundi lake la damu ni ...........................................................................*

10. *Malalamiko mengine yoyote anayotoa mwanafunzi kuhusu afya au viungo vyake*

    ..........................................................................................................................................

11. *Kuna tatizo au ugonjwa kuhusiana na afya yake linaloweza kufanya mwanafunzi huyu alazimie kusoma shule iliyo karibu na hospitali ya wilaya au mkoa?*

    ..........................................................................................................................................

12. *Maoni na mapendekezo ya daktari apokelewe au asipokelewe kuendelea na masomo ya shule ya sekondari mwaka Huu:*

    ........................................................................................................

| | | |
|---|---|---|
| ........................ | ........................ | .................... |
| *J ina kamili la Mganga* | *sahihi yako* | *Cheo* |

| | |
|---|---|
| .................... | .................. |
| ***TAREHE*** | ***MUHURI*** |

6

# OFISI YA RAIS-TAMISEMI
# HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI
# SHULE YA SEKONDARI KIRANDO

**MKATABA**

Unashauriwa kujaza fomu hii ya mapatano kikamilifu

**SEHEMU A:MWANAFUNZI**

Mimi…………………………………………………………………..Nimesoma na kuelewa vizuri sheria,maagizo na kanuni zote za shule,nakubali/sikubali nafasi hii na kuwa nitatumia uwezo wangu wote na kujiendeleza kitaaluma,nitatii sheria,maagizo na kanuni zote za shule na wala sitashiriki katika mgomo,fujo na makosa yoyote ya jinai.

**SAHIHI……………………………**

**TAREHE…………………………………………Bandika picha ya passportsize hapa**

**SEHEMU B:MZAZI/MLEZI**

Mimi………………………………………………………………..Mzazi/mleziwa……………… …………………………..Nimepokea taarifa ya mwanangu ya kujiunga na shule ya sekondari Kirando.Kwa kutambua umuhimu wa Elimu na wajibu wangu,naahidi kuw amuda wote mwanangu atakapokuwa shuleni nitashirikiana na uongozi wa shule kumlea kwa kufuata sheria,maagizo na kanuni zote za shule na kuhakikisha kuwa anahudhuria masomo kwa kadri ya ratiba ya shule,nitatekeleza maelekezo yatakayotolewa na shule.


**SAHIHI……………………………**

**TAREHE……………………………….**

**NAMBA ZA SIMU……………………**

**MAHALI ANAPOPATIKANA…………………**







NYEUSI